NAMBARI YA MTAHINIWA ___________________

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA DARASA LA NNE

121 KISWAHILI

MUDA: SAA 2.00 JUMATATU 25 NOVEMBA, 2019 MCHANA

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Swali MOJA (1) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu YOTE yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 13 zenye maandishi



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

# SEHEMU A: (Alama 20)

## UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Sungura aliwadanganya wenzake kwa kipindi kirefu. Alitumia ujanja wake kuwafanya wenzake <u>wajinga</u>. Alisababisha wengi wapigwe na wakati mwengine hata <u>kupoteza maisha</u>. Siku moja wanyama waliitisha mkutano ili kila mmoja atoe malalamiko yake. Katika mkutano wao, wanyama wote walikubaliana kumkomesha sungura kwa ujanja wake.

Mnyama aliyeteseka zaidi alikuwa ni fisi ambaye alidanganywa kwamba mkono wa binadamu ungeanguka. Mara nyingi fisi alimfuata binadamu lakini aliambulia <u>kipigo cha kumvunja mbavu</u>. Fisi alipata <u>majeraha</u> makubwa kutokana na kipigo alichokipata. Wanyama wote walimsikitikia sana fisi.

Zaidi ya hayo, sungura hakuwa na mashirikiano mazuri na wenzake, alikataa kushiriki katika kazi ya uchimbaji wa kisima cha maji na badala yake akaendelea kuiba maji msimu wa ukame. Wanyama wote kwa pamoja waliamua ni heri sungura afe. Fisi, chui na simba waliahidi kuongoza msafara mpaka <u>wamtie sungura mikononi</u>.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

1. Maswali

i. Kwa kipindi gani sungura aliwadanganya wenzake?

______________________________________________

______________________________________________

ii. Sungura alitumia ujanja wake kwa lengo gani?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

iii. Bainisha tabia mbili (2) mbaya alizokuwanazo sungura.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

iv. Wanyama waliamua nini katika mkutano wao?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

v. Unadhani kwa nini wanyama wote walimsikitikia sana fisi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Toa maana ya neno au kifungu cha maneno kilichopigiwa mstari.

SEHEMU B: (Alama 40)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.

Kwa mfano:

i. Mwizi amekamatwa.

_N____________________

ii. Yule ndiye mkorofi.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

iii. Mwanafunzi <u>hodari</u> amepewa zawadi.

_______________________________________________

iv. <u>Wewe</u> ni rafiki yangu.

_______________________________________________

v. Ameruka <u>mara tatu</u>.

_______________________________________________

vi. Watoto wote <u>wanasoma</u> vizuri.

_______________________________________________

4. Toa kinyume cha maneno yafuatayo:
Nambari moja imetumika kama mfano.

| | NENO | KINYUME |
|---|---|---|
| i. | Nenda | Rudi |
| ii. | Mbovu | |
| iii. | Rafiki | |
| iv. | Cheka | |
| v. | Amani | |
| vi. | Funga | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

5. a) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

i. 1,100

_______________________________________________

_______________________________________________

ii. 98,888

_______________________________________________

_______________________________________________

iii. 362,045

_______________________________________________

_______________________________________________

b) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i. Elfu moja na arubaini na mbili.

_______________________________________________

ii. Laki nne, elfu hamsini, mia tano na hamsini na tano.

_______________________________________________

6. a) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiingereza.

i. Bendera yetu ina rangi nzuri.

_______________________________________________

_______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

ii. Embe na ndizi ni matunda matamu.

______________________________________________

______________________________________________

iii. Tulinunua vijiko kumi na nane na uma mmoja.

______________________________________________

______________________________________________

b) Eleza umuhimu wa vitu vifuatavyo:

i. Chandarua

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

ii. Miti

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C: (Alama 20)

## FASIHI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

7. Tunga hadithi fupi inayotoa ujumbe "Umoja ni Ushindi".



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

8. a) Eleza mafunzo ya methali zifuatazo:

i. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

ii. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

iii. Mwenda pole hajikwai.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

b) i. Nini maana ya ngonjera?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

ii. Orodhesha vipengele vinne (4) muhimu vya ngonjera.

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D: (Alama 20)

## UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

9. Andika kadi ya mwaliko kwa rafiki yako, umualike katika sherehe ya maulid ya kuzaliwa kwa ndugu yako.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

10. Taja vipengele vyote muhimu vya uandishi wa barua ya kawaida.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

====================



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org